**MWITO PROG 1116 KISWAHILI SCRIPT**

**SCRIPTURE:ROMANS 7:7**

**TRANSWORLD RADIO**

**INTRO-:**

Nakuksaribisha msikilizaji wazngu mpendwa kukisikiliza kipindi cha MWITO ambacho ni cha mafundisho na kinachoandaliwa na TransWorld Radio,Nairobi.Madhumuni ya kipindi hiki ni kukusaidia kulielewa neno la Mungu kwa undani kupitia hudum ya mtume Paulo jinsi itakavyoainishwa kwenye kitabu cha Warumi.Na ikiwa hukuwa nasi juma lililopita nitakupatia muhtasari wa somo lililopita kisha tuendelee.Lakini kabla ya hapo nakufahamisha kuwa unaweza kujipatia nakala ya agano jipya la Bibilia ikiwa utatuandikia na kutufahmisha kuhusu ushiriki wako kwenye vipindi vyetu vya Transworld radio na idhaa zetu tunakosikika kutoka Voi,Lamu,Marsabit,Lodwar n Turkana.Lngoltu ni kueneza neno la Bwana kwa kila jamii humu nchini.

Somo lililopita lilizingatia aya ya 7.Leo pia tutadumu kwenye aya iyo hiyo.Na tusome aya hiyo ndipo tuendelee na somo la leo……..….***Tuseme basi? Torati ni dhambi? Hasha walakini singelitambua dhambi ila kwa sheria kwa kuwa singalijua kutamani kama torati isingalisema,usitamani.Lakini dhambi ilipata nafasi kwa ile amri ikafanya ndani yangu kila namna ya kutamani.Kwa maana dhambi bila sheria imekufa.***

Naam mpendwa msikilizaji somo leo tutajumuisha aya za 7,8 na 9 za Warumi sura ya 7.Nnamini kuwa umepata angalau muhtasari wa mhala tulipoachwa kwene kipindi kilichopita.Ningependa sasa tusome kuanzia aya ya 8 hadi 9 ya Warumi 7.***Lakini dhambi ilipata nafasi kwa ile amri ikaffanya ndai yangu kila namna ya kutamani.Kwa maana dhambi bila sheria imekufa.Nami nalikuwa hai hapo kwanza bila sheria ila iipokuja ile amri,dhambi ilihuika,nami nikafa.***

Naam Mungu alijua kuwa dhambi ilikuwepo na alitaka kitu cha kuitia uhai ili sheria ipate uhai ndipo binadamu ambao hawana uhusiano wa moja kwa moja na Muumba wao wajipime kwa

sheria hiyo.Sheria ilitumika kama kibainiho cha jinsi dhambi ilivyokuwa imeathiri binadamu.

Kwenye aya ya 9…***mtume Paulo anasema Nami nalikuwa hai hapo kwanza bila sheria ila iipokuja ile amri,dhambi ilihuika,nami nikafa.***Hapa mtume Paulo anaturegesha nyuma nyskati zake ambapo alizaliwa tu kama binadamu wengine,lakini baadaye katika maisha akaangaziwa alipokuwa njiani kwenda Damesiki kuwatesa  wakristo.Paulo ananukuu maneno ya Daudi ambaye alisema binadamu huzaliwa akisema uwongo na tena katika dhambi.Kwamba wanazaliwa na dhambi ya urithi ya Adamu.Hali hiyo huendelea hadi wanapofikia ufahamu wa mema na mabaya ambapo yatgemea umri na mazingira.Hakuna kiwango cha miaka.Yaweza kuwa mtoto akiwa na miaka 12 au hata 20.Au hata yaweza kuwa miaka mitano!

Kuna baadi ya watoto ambao huzaliwa katika mazingira ambayo hutakiwa kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu.Wengine huhusishwa kwenye mipango ya watoto ya kikristo nyumbani na hata kanisani.Baadhi yao haya wamempokea Kristo kuwa mwokozi wao wakiwa na umri wa miaka michache.Siwezi kuweka umri ambapo waoto humpokea Kristo kuwa mwokozi

wao.Nimehudumu katika jamii zinazoishi maisha duni katika sehemu mbali mbali za ulimwengu,ambapo hata ni vigumu kupata watoto wadogo wanaomwamini Kristo kuwa mwokozi wao wakiwa na umri mdogo.Yaani wakati ambapo anawajibika kwa Mungu.Lakini kwa ujumla tunaweza kusema labda wengi wa watoto kama hao huwa na uhusiano wa mapema na Mungu wakiwa na umri wa kati ya miaka 7 hadi 10.Kupitia watoto kama hao majirani huja kutambua kuwa kuna kitu wanakosa katika misha yao.Kwa njia ya ushuda wanafahamu kuwa kuna kitu wanakosa maishani mwao.

Na hiki ndicho mtume Paulo alikuwa akifanya.Alisema kwamba wakati mmoja hakuwa akiongozwa na sheria na huo ilikuwa enzi ya maasumu au ya kutokuwa na hatia.Hiki ni kipindi ambapo watoto hawajafikia umri wa kujua mema na mabaya,kwa hivyo wajapokuwa na dhambi ni zile ambazo hawakuzitenda kimaksudi.Mtume Paulo anaturejesha Yuma na kusema kwamba wakati akuwa chini ya sheria ule utu wa kale ulimshurutisha kuasi na kutenda kinyume cha yale alioamriwa kutenda au kinyume cha desturi ya maisha.Kwa hivyo wakati mtume Paulo anaposema kwenye aya ya 10 kwamba…***nikaona ile amri***

***iletayo uzima ya kuwa kwangu mimi ilileta mauti'***…hii inamaanisha kama angalidumisha basi angekufa kwa torati na ukweli ungekuwa kiyume chake.Yaani ukifa kwa torati ,utapata uzima wa milele.Sote twajua kuwa mshahara wa dhambi ni mauti.Lakini ndugu yangu Mungu ni mwenye rehema nyingi;angependa uwe na uhusiano wa moja kwa moja naye kupitia mwanawe Yesu kristo.Je utamfungulia mlango wa moyo wako aingie?Umeokoka?

Mungu alitaka tujue ubatili wa sheria na jinsi tunavyoweza sasa kumkimbilia mwokozi Yesu.Ikiwa hujawahi kumwamini huyu Yesu kristo,wakayi ni huu.Anahitaji maisha yako akuokoe.Je? Una uhudiano wa moja kwa mja na mwokozi wako?

Chukua fursa hii adhimu na utende unalostahili kutenda ili usitahyari siku ya mswisho, wakati majina ya watakatifu yatakapoitwa na lako lisikose kuwapo na uepuke hali ya kutengwa na kurushwa huko Jehanamu kulipo na kusaga meno na vilio.Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1116 Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia nambari nitakayokupatia muda mfupi ujao. Tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road,

baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Nitumie arafa yako kwa nambari hii -0721 970 520. Au nipigie simu kwa nambari-:020 2679842 Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya 8 sura ya 7 ya kitabu cha Warumi.Ni mimi ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mibaraka na neema tele zake zake Mungu.Bwana akubariki na udumu katika neema yake.Kwaheri.

…………………………….TAMATI…………………..